## Maswali

1. Nani walikuwa wakipigana na Waisraeli?
2. Jina la jitu liliitwa nani?
3. Goliathi aliwapa Waisraeli changa moto wafanye nini?
4. Sauli aliahidi nini kwa mtu yeyote atakayepigana na Goliathi?
5. Daudi aliambia Sauli nini?
6. Mbona Sauli aliona kwamba Daudi hangeweza kupigana na Goliathi**?**
7. Mungu alikuwa amesaidia Daudi namna gani alipokuwa mchungaji?
8. Daudi aliambia Goliathi nini?
9. Daudi aliuwa Goliathi namna gani?
10. Nani alisaidia Daudi kuua Goliathi?

## Majibu

1. Wafilisti walikuwa wakipigana na Waisraeli.
2. Jitu liliitwa Goliathi.
3. Goliathi aliwapa Waisraeli changa moto ya kumpa mtu wapigane naye.
4. Sauli aliahidi kutoa mali na bintiye kuwa mkewe.
5. Daudi alisema kwamba atapigana na Goliathi.
6. Sauli alisema kwamba Daudi alikuwa kijana tu. Hakukuwa na ujuzi wa kupigana.
7. Mungu alisaidia Daudi kuua simba na dubu wakati alikuwa mchungaji.
8. "Unakuja kupigana na mimi kwa upanga. Ninakuja kwako kwa Jina la Mungu."
9. Daudi alilinga jiwe likapiga na likabumbuaza Goliathi.Aliua Goliathi kwa upanga wake alipomkata kichwa chake.
10. Mungu alisaidia Daudi kuua Goliathi

## SHULE YA JUMAPILI YA CBM

### Awamu ya 2 Mwaka wa 2

# 60 Daudi na Goliathi

## Kwa Biblia

1 Samweli mlango wa 17

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Daudi alikuwa na nguvu kwa sababu alikuwa na imani kwa Mungu

## Somo

Wafilisti walianza kupigana na Waisraeli tena. Wafilisti walipiga kambi kwa kilima moja. Waisraeli nao walipiga kambi kwa kilima kingine mbele kwa hivyo kukawa na bonde katikati yao. Ndugu wa tatu wa Daudi walipigana kwa jeshi la Sauli.

Siku moja Yese baba wa Daudi, alileta Daudi kutoka vilimani alikokuwa akichunga kondoo. Yese alimpa Daudi chakula. Alimwambia awapelekee ndugu zake watatu chakula. Yese alimwambia akienda aangalie vile nduguze walikuwa wakiendelea na vile vita. Daudi aliendа kwa kambi ya Waisraeli. Wanajeshi hawakuwa wakipigana Daudi alipowasili. Daudi aliacha chakula na mtu anayelinda vifaa na kuenda kuona nduguze.

Goliathi, jitu mkubwa alitokea kwa kambi ya Wafilisti. Goliathi alikuwa zaidi ya kimo cha futi tisa kwa urefu. Alikuwa na nguvu nyingi sana. Mavazi za vita za chuma alizovaa zilikuwa nzito. Panga na mkuki alizobeba zilikuwa kubwa mno. Goliathi alitoa sauti kutoka upande mwingine wa bonde. Goliathi aliwapa Waisraeli changa moto akisema, "Chagua mtu aje tupigane. Akiniua basi, Wafilisti watakuwa watumishi wenu. Lakini nikimua, nyinyi mtakuwa watumishi wa Wafilisti. Chagua mtu aje tupigane na yeye."

Waisraeli wote walitishika sana. Hakuna aliyekuwa hodari kupigana na jitu kubwa kama Goliathi. Lakini Daudi hakuogopa. Alikuwa na imani kwa Mungu.

Daudi aliamini kwamba Mungu anaweza kurahihisha kinachoonekana kigumu kwa binadamu. Goliathi alifanyia watu wa jeshi la Mungu msaha. Daudi alishangaa sana kuona Waisraeli wote wametishika na kuogopa. Alishangaa kuona kwamba hakuna hata mtu mmoja aliyekuwa na ujasiri wa kuamini Mungu ili apigane na Goliathi.


Mfalme Sauli hakuwa na ujasiri wa kupigana na Goliathi. Sauli aliahidi kutuza mtu yeyote atakayepiga Goliathi. Yeyote atakayekuwa hodari na apige Goliathi, Sauli aliahidi kumpa mali na bintiye awe mke wake.



Daudi alimwendea Mfalme Sauli na kumwambia, “Nitaenda nipigane na Goliathi.” Daudi alikuwa kijana mdogo. Hakukuwa na umri wa kuwa kwa jeshi la Sauli. Hakukuwa na ujusi wa kupigana. Sauli alimjibu, “Hauwezi kupigana na hili jitu. Wewe bado kijana.”

Daudi aliambia Sauli kwamba yeye anaamini kwa nguvu za Mungu. Daudi alipokuwa akichunga kondoo, wakati mwingine simba au dubu angekuja na kuchukua kondoo. Daudi aliua simba au dubu na kuponya kondoo. Daudi aliamini Mungu. Mungu alikuwa amesaidia Daudi kuua simba na dubu. Daudi aliambia Sauli, “Niliua simba na dubu. Hili jitu la Wafilisti litakuwa kama hao, kwa sababu ya kudharau jeshi la Mungu aishie.”

Daudi aliamini Mungu. Daudi aliamini kwamba Mungu atamsaidia aue Goliathi, aliyekuwa amedharau jeshi la watu wa Mungu.



Kwa hivyo Sauli alikubali na akamwambia Daudi, “Enda na Mungu awe nawe.” Sauli alipea Daudi mavazi zake za chuma na upanga. Daudi alivaa hizo mavazi za Sauli. Lakini hakukuwa amezoea kuvaa mavazi za chuma. Hakujisikia vizuri. Kwa hivyo alizitoa. Aliambia Sauli, “Sitavaa mavazi zako za chuma, sijazoea.”

Daudi aliendа kupigana na Goliathi. Alichukua mkononi mwake fimbo yake ya uchungaji. Alichukua mfuko wake na kombeo. Daudi alisimama kwa kijito kilichokuwa bondeni na kuchukua mawe laini matano. Aliweka hayo mawe kwa mfuko wake.

Goliathi alikuja kukutana na Daudi. Alivaa mavazi mazito ya vita. Mbele yake kulikuwa na mtu aliyembebea silaha. Goliathi alikuja kupigana na Daudi. Goliathi alipoona kwamba Daudi ni kijana mdogo, alikasirika sana. Alipaza sauti na kusema, “Unafikiri kwamba mimi ni mbwa? Mbona unakuja kupigana na mimi kwa vijiti na mawe? Kuja hapa na nyama yako nitawapa ndege wa angani na wanyama wa mwituni.”

Daudi alijibu Goliathi kwa sauti, “Unakuja kupigana na mimi kwa upanga na mkuki. Lakini nakuja kupigana na wewe kwa Jina la Bwana Mungu wa majeshi ya Israeli. Leo hii Mungu atakutia mkononi mwangu. Nitakupiga chini na kutoa kichwa chako. Hapa ndio kila mtu atajua kwamba kuna Mungu katika Israeli.”



Wafilisti walisongea Daudi ili wamshambulie. Daudi alikimbia mbele aende akutane na Goliathi. Aliweka jiwe ndani ya kombea lake na akarushia Goliathi. Jiwe lilipiga Goliathi kwa paji la uso na akaanguka chini kifudifudi.

Jiwe kutoka kwa kombeo lilimbumbuaza Goliathi. Halafu Daudi akachukua upanga wake akamua na akatoa kichwa. Wafilisti walipoona Goliathi amekufa, walitoroka. Waisraeli walifukuza Wafilisti na kuwaua. Daudi alichukua kichwa cha Goliathi na kupelekea mfalme Sauli.

Baadaye wanawake waliimba nakucheza kwa furaha kwa sababu ya kushinda Wafilisti. Waliimba wakisema, “Sauli amewaua elfu zake, na Daudi makumi elfu yake.” Sauli aliposikia huo wimbo, alikasirika sana. Alionea Daudi wivu.